

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



23 JUNI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA TISA – 23 JUNI, 2016

I. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

II. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

419. MHESHIMIWA OMAR MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Ili kuleta ufanisi wa kimaendeleo na kusogeza karibu huduma za kijamii kwa Wananchi, Serikali hugawa Wilaya na Majimbo kwa kuangalia ukubwa wa eneo, idadi ya watu kwenye eneo husika pamoja na shughuli za kiuchumi na Wilaya ya Kilindi ni mionganini mwa Wilaya chache zinazozalisha mazao ya Kilimo na biashara kwa eneo kubwa:-

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuligawa Jimbo hilo lenye ukubwa wa mita za mraba 6125.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

420. MHESHIMIWA DKT. ELLY MARCO MACHA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kufuatia mpango wa Serikali wa utoaji wa elimu bure kuanzia Elimu ya Msingi hadi Sekondari na kwamba watu wenyewe ulemavu wanakabiliwa na umaskini uliokithiri na hivyo kushindwa kumudu gharama za elimu:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kutoa elimu bure kwa wanafunzi wenyewe ulemavu kwa ngazi ya kidato cha tano na cha sita;
- (b) Je, Serikali inaweza kulihakikishia Bunge hili kwamba itaweka utaratibu mzuri wa usafiri na huduma nyingine muhimu za kuwawezesha wanafunzi wenyewe ulemavu kupata elimu katika shule wanazopangiwa;
- (c) Je, Serikali inaweza kulithibitishia Bunge hili kwamba wanafunzi wenyewe ulemavu wanaoingia Vyuo Vikuu watapewa kipaumbele katika kupata mikopo bila usumbufu wowote.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

421. MHESHIMIWA SIXTUS RAPHAEL MAPUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mji wa Mbinga ni mionganini mwa Miji inayokua kwa kasi hapa nchini hali inayopelekea ongezeko la hitaji kubwa la huduma ya maji safi na salama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mradi wa uhakika wa maji safi na salama utakaoweza kuwashudumia Wananchi wa Mbinga.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

422. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa ardhi kati ya Wananchi wa Malangali ndani ya Wilaya ya Wanging'ombe na Wafanyakazi wa Hifadhi ya Mpanga.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

423. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Serikali imekuwa ikitoa huduma za dawa bila malipo kwa baadhi ya maradhi kama vile UKIMWI, TB nk:-

- 
- (a) Je, ni maradhi ya aina gani yaliyo katika orodha ya kupatiwa dawa bila malipo;
 - (b) Je, ni kwa kiasi gani Serikali imefanikiwa kufikia malengo katika mpango huo wa kusaidia Wananchi kupata dawa hizo.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

1. Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wa Mwaka 2016 (The Access to Information Bill, 2016).
2. Muswada wa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini wa Mwaka 2016 (The Valuation and Valuers Registration Bill, 2016).

- 
3. Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016 (The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016).
 4. Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 (The Chemist Professionals Bill, 2016).

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2016 (*The Finance Bill, 2016*).

DODOMA
23 JUNI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE